# Marine Services Company Limited (MSCL)

## Taarifa ya Kampuni ya Huduma za Meli – MSCL Kuhusu Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara

Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services Company Limited – MSCL) ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni sura 212 mnamo tarehe 08/12/1997 kutokana na kilichokuwa kitengo cha usafirishaji wa majini cha Shirika la Reli (TRC).

Baada ya kuanzishwa kwa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), mali zote zilizokuwa chini ya kitengo cha usafiri majini cha TRC zilihamishiwa katika Kampuni hii mpya mnamo tarehe 21/06/1999 kupitia Gazeti la Serikali No. 125A. Kampuni ilianza kazi tarehe 01/08/1999 ikiwa na mtaji wa meli 15 bila fedha yoyote.

Kampuni iliendelea kufanya kazi huku ikimiliki meli, bandari zote na miundombinu yake yote katika maziwa makuu hadi tarehe 30/06/2006. Mnamo mwaka 2004, serikali ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kupitia sheria No. 17 ya 2004. Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Bandari ilianza kutumika tarehe 01/07/2006.

Kutokana na mabadiliko haya baadhi ya mali za Kampuni ya Huduma za Meli ikiwemo miundombinu yote ya kibandari, meli moja, majengo ya ofisi, karakana na vyelezo katika maziwa yote makuu vilihamishiwa Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mabadiliko haya yalipunguza ukubwa na mali za Kampuni pamoja na baadhi ya vyanzo vyake vya mapato.

Kampuni hii kwa sasa inaendesha jumla ya meli 14 za abiria na mizigo, ambapo meli 9 ziko ziwa Victoria, 3 ziko ziwa Tanganyika na 2 ziwa Nyasa. Idadi hii ni baada ya meli moja kuhamishiwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Jedwali Na. 9.3 inaonesha meli hizo kwa kila ziwa.

Kampuni hii inaundwa na Matawi matatu yaani Tawi la Mwanza katika Ziwa Victoria; Tawi la Kigoma katika Ziwa Tanganyika na Tawi la Kyela Katika Ziwa Nyasa. Makao Makuu ya Kampuni yako Mwanza.

**Majukumu ya Kampuni**

Shughuli kubwa za Kampuni hii ni kusafirisha abiria na mizigo katika maziwa yote matatu, ikitoa huduma kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya mwambao wa maziwa haya na katika visiwa, ndani ya nchi na nje ya nchi.

Vile vile Kampuni hii ni daraja katika shughuli za kibiashara na kijamii kati ya Tanzania na nchi jirani. Nchi za Uganda na Kenya katika Ziwa Victoria, Burundi, Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia katika Ziwa Tanganyika, na Malawi katika Ziwa Nyasa.

Kutoa huduma bora, inayotegemewa, inayoaminika, inayotabirika, angalifu na yenye kujali usalama kwa wateja wake katika maziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Kuwa kampuni ya usafirishaji katika maziwa iliyo na ushindani, yenye kutegemewa, salama na itendayo kwa kuwalenga wateja wake siku zote.

Kufanya matengenezo ya mara kwa mara (preventive/routine maintenance) ya meli zake kufuatana na miongozo iliyopo katika "Merchant Shipping Act". Kuboresha usalama wa abiria kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kuokolea maisha melini vinatosheleza mahitaji kulingana na idadi na wafanyakazi walioko melini.

Kampuni hii inaendelea kutekeleza makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi (UNHCR) kwa kurudisha nyumbani Wakimbizi wa DRC toka Kigoma, Tanzania na Mpulungu, Zambia kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Zoezi hili bado ni endelevu.

**Jedwali Na. 1: Uwezo wa Kila Meli na Mwaka wa Ujenzi kabla na Baada ya Uhuru**

| Jina la Meli | Uwezo wa Ubebaji | |
|---|---|---|
| | **Abiria** | **Mzigo (Tani)** |
| **ZIWA VICTORIA** | | |
| M.V. Victoria | 1200 | 200 |
| M.V. Butiama | 200 | 100 |
| M.V. Serengeti | 593 | 350 |
| M.V. Clarias | 293 | 10 |
| M.T. Nyangumi | - | (Mafuta) 350 |
| M.T. Ukerewe | - | 480 |
| M.L. Maindi | - | 120 |
| M.L. Wimbi | - | 120 |
| M.V. Umoja | - | 1200 |
| **ZIWA TANGANYIKA** | | |
| M.V. Liemba | 600 | 200 |
| M.V. Mwongozo | 800 | 80 |
| M.T. Sangara | - | (Mafuta) 350 |
| **ZIWA NYASA** | | |
| M.V. Iringa | 139 | 5 |
| M.V. Songea | 212 | 50 |

### Malengo ya Kampuni

i. Kujiendesha kwa uwezo wote tulio nao ifikapo mwaka 2013,
ii. Kutoa huduma zenye ongezeko la thamani,
iii. Kuajiri na kubakiza watumishi stadi katika soko la sasa,
iv. Kuongeza mapato ya shughuli kwa zaidi ya 50% ifikapo mwisho wa mwaka 2013.
v. Kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kwa usalama, uhakika na kwa bei nafuu.
vi. Kuwekeza kwenye miradi ambayo inalenga kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha huduma.

### Hali ya Uongozi na Utawala Kuanzia 1961

1976: Idara ya Usafirishaji Majini ilikuwa chini ya Mkurugenzi wa Usafirishaji Reli ambayo makao makuu yake yalikuwa Nairobi – Kenya na hapa Tanzania upande wa usafirishaji

majini kitengo kilikuwa chini ya Mrakibu Usafirishaji (District Traffic Superintendent – Mwanza) kitengo cha “Marine Transport Officer – Mwanza” (Mwanza na Kigoma).

1977: Baada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika kitengo cha Usafirishaji majini kilibaki kikiendeshwa na Ofisi iliyokuwa ya Meneja Usafirishaji (CTM) chini ya Warakibu wa Usafirishaji (Mwanza na Tabora) chini ya Marine Transport Officer (MTO) Mwanza.

1977: Meli zilizokuwa za Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Railways) Ziwa Victoria nyingi zilikamatwa zikabaki nchini Kenya – Kisumu nazo ni M.V. Victoria, M.V. Umoja, M.T. Nyangumi, M.S. Usoga, M.V. Uhuru na nyinginezo nyingi.

Meli tulizobaki nazo upande wa Tanzania Ziwa Victoria ni M.V. Clarias, M.S. Buvuma na M.V. Ng’ombe na S.S. Buganda. Kwa Ziwa Tanganyika tulibaki na meli ya S.S. Liemba ikiwa kwenye matengenezo makubwa ya kubadilishwa kutoka injini za mvuke (steam engine) kuwekewa injini za mafuta (Diesel Engine). Kazi ilikamilika mwaka 1978 na kuanza kazi ya kuhudumia wananchi wa mwambao wa Ziwa Tangnyika kwa upande wa Tanzania na baadaye wananchi wa nchi za jirani za Burundi, Zaire (DRC) na Zambia.

1978: Kurudishwa kwa meli 3 kutoka Kenya ambazo ni M.V. Victoria, M.T. Nyangumi na M.V. Umoja.

1979: Ndiyo ujenzi wa meli zilizotoka Ubelgiji ulipoanza. Meli hizo ni: M.V. Bukoba ilijengwa mwaka 1979, M.V. Butiama na M.T. Sangara zilijengwa mwaka 1980, M.V. Mwongozo mwaka 1982 na M.T. Ukerewe mwaka 1983.

Kitengo cha uendeshaji meli, kwenye maziwa haya matatu (3); Ziwa Nyasa, Tanganyika na Victoria ziliwekwa chini ya Meneja Usafirishaji. Reli (CTM) kwa kuunda matawi matatu. Tawi la Mwanza chini ya cheo kipya kilichojulikana kama Engineer Incharge – Lake Victoria, hivyo hivyo ilikuwa kwa vituo vya Kyela na Kigoma.

1982: Shirika la Reli lilipata udhamini wa uendeshaji wa meli katika maziwa kutoka Denmark kupitia DANIDA.

Uundwaji wa kitengo cha usafirishaji majini kiliondolewa kwa Meneja Usafirishaji (CTM) Reli na kuanzishwa Idara iliyojulikana kama TRC MARINE DIVISION chini ya Chief of Marine Operations (CMO), ambaye aliwajibika kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli.

1983: Zilizokuwa meli za TACOSHILI Ziwa Nyasa zilikabidhiwa Shirika la Reli kwa kuziendesha na miundombinu yake yote. Meli hizo ni M.V. Iringa na M.V. Songea.

1988: Pamoja na hayo yote kufanyika chini ya msaada wa DANIDA, yaliundwa matawi matatu ambayo ni Mwanza, Kigoma na Kyela chini ya uongozi wa District Marine Manager na vitengo kama vile Karakana, Ugavi na mengineyo. Makao makuu yakiwa Dar-es-salaam. Katika kipindi hicho meli za M.V. Serengeti na M.T. Linda zilijengwa kwa msaada wa DANIDA. Pia, katika kipindi hicho meli za M.V. Victoria na M.V. Liemba zilifanyiwa matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja na kuwekewa mitambo mipya.

1996: Kampuni ya Huduma za Meli (Marine Services Company Limited – MSCL) ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni sura 212 mnamo tarehe 08/12/1997 kutokana na

kilichokuwa kitengo cha usafirishaji wa majini cha Shirika la Reli (TRC). Kutenganisha Shirika la Reli na kitengo cha usafirishaji wa majini na kuanzishwa Kampuni mpya ya Huduma za Meli ilikuwa ni mwanzo wa utekelezaji wa mkakati wa ubinafishwaji wa taasisi hizo mbili.

Baada ya kuanzishwa kwa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), mali zote zilizokuwa chini ya kitengo cha usafiri majini cha TRC zilihamishiwa katika Kampuni hii mpya mnamo tarehe 21/06/1999 kupitia Gazeti la Serikali No. 125A. Kampuni ilianza kazi tarehe 01/08/1999 ikiwa na mtaji wa meli 15 bila fedha yoyote.

Kampuni iliendelea kufanya kazi huku ikimiliki meli, Bandari zote na miundombinu yake yote katika maziwa makuu hadi tarehe 30/06/2006. Mnamo mwaka 2004, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Bandari kupitia sheria No. 17 ya 2004. Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Bandari ilianza kutumika tarehe 01/07/2006.

Mara tu baada ya uhuru wa Tanzania, sera ilikuwa ni Serikali kuendesha na kusimamia usafiri wa majini katika maziwa makuu. Sera hiyo iliendelea hadi mwaka 1995 ambapo Serikali ilijitoa kabisa katika shughuli za biashara na hivyo kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji binafsi kuwekeza katika shughuli mbalimbali za kibiashara zikiwemo usafiri wa majini.

Serikali imeweka mazingira mazuri na inakaribisha wawekezaji toka nje ya nchi na ndani ya nchi kuwekeza katika eneo hili, yaani kununua meli nzuri zaidi ambazo zitakidhi vyema mahitaji ya wasafiri katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Shughuli kuu ya MSCL ni kutoa huduma ya usafirishaji majini kwa abiria na mizigo katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Vile vile hujishughulisha na utengenezaji na utunzaji wa vyombo vyake. Katika kutekeleza shughuli zake za kudhibiti na kiutawala, MSCL imekuwa ikiweka maanani yafuatayo:

i. Malengo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

ii. Kipengele cha wajibu wa huduma kwa umma (Public Service Obligation) kwa watu waishio kuzunguka maziwa hayo matatu ambao hawana njia mbadala za usafiri, hususani, kuzunguka Maziwa ya Tanganyika na Nyasa, ambako huduma za usafiri ni chache.

iii. Usalama, afya na ustawi wa jumla wa umma kwa kufanya shughuli zake katika njia ambazo zinalinda mazingira kwa taratibu zilizofungamana na endelevu.

Tanzania imepitia mifumo miwili ya kisiasa tangu mwaka 1961. Mara tu baada ya uhuru tulikuwa na mfumo wa ujamaa. Katika kipindi hicho meli zilitoa huduma kwa hasara na serikali ilifidia hasara hiyo.

Katika ulinzi, meli zimetoa michango mbalimbali katika ulinzi wa nchi. Kwa mfano, meli ya M.V. Victoria ilisafirisha zaidi ya wanajeshi 2,000 wa Tanzania kutoka Mwanza kwenda Uganda katika Ziwa Victoria ili kufanikisha vita ya kumuondoa madarakani nduli Idd Amin. Meli hii pia ilitumika kuwarudisha wanajeshi Tanzania.

Meli ya M.V. Umoja ilisafirisha vifaa vya kijeshi kama vile vifaru na wanajeshi kwenda Uganda wakati vya vita hivyo. Pia meli ya M.T. Nyangumi ilisafirisha mafuta ya kuendeshea vifaa mbalimbali wakati wa vita hivyo.

Katika kipindi hiki cha soko huria, Kampuni imekuwa ikijiendesha kibiashara kwa kutumia mapato yanayotokana na usafirishaji wa abiria na mizigo.

**Mafanikio Yaliyopatikana Hadi Sasa**

i) Kampuni imeendelea kuzifanyia matengenezo makubwa na yale ya kawaida meli ambazo ni chakavu.
ii) Kampuni imeendelea kusafirisha abiria na mizigo katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwa usalama, uhakika na gharama nafuu.
iii) Kampuni imeendelea kufanya ukarabati mkubwa (Rehabilitation) na kuboresha hali ya meli zake ili kuziongezea maisha na uhakika wa kufanya safari zake salama.
iv) Kuongeza na kuimarisha hali ya usalama wa meli zake kwa kuboresha vifaa vya usalama, kusisitiza uangalifu wa utendaji kazini, kuepusha ulevi na kuelimisha wananchi (wasafiri) matumizi sahihi ya vifaa vya usalama ndani ya meli zetu.
v) Kuzifanyia ukaguzi kila mwaka kupitia Mkaguzi wa Serikali na kufuata miongozo ya Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA) kwa uendeshaji salama.
vi) Kampuni imekuwa ikiziwekea bima meli zote dhidi ya matukio yoyote yasiyotarajiwa ikiwa ni pamoja na abiria na mizigo pamoja na wafanyakazi melini.
vii) Kupanua soko la meli za Kampuni kupitia matangazo redioni na katika majarida mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.
viii) Kukuza na kuboresha huduma kwa wateja (Customer Care) ambao ndiyo msingi wa kuboresha soko.
ix) Uongozi wa Kampuni kwa kutambua kuwa uwezo wa serikali kugharamia miradi yote una ukomo, tuliandaa andiko la mradi wa ukarabati wa meli za Kampuni na ujenzi wa meli mpya na kulisambaza kwa washirika wa maendeleo (development partners).

Serikali ya Denmark, kupitia Shirika lake la maendeleo "DANIDA" ilionyesha utayari kutoa fedha za kugharamia mradi na tayari upembuzi yakinifu umefanyika na ripoti yake iko kwenye hatua za mwisho. Aidha, serikali ya Ujerumani imeonyesha utayari wa kugharamia matengenezo makubwa ya kuboresha meli ya M.V. Liemba.

## Changamoto

Kampuni ya Huduma za Meli inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:
i) Meli nyingi kuwa za zamani sana na kuwa chakavu na hivyo kuchukua sehemu kubwa ya mapato yapatikanayo katika kufanya matengenezo ya mara kwa mara na pia kusababisha ongezeko la matumizi ya mafuta.
ii) Kupanda kwa bei za vipuri vinavyohitajika kuzifanyia matengenezo meli zetu ambavyo vinapatikana nje ya nchi.
iii) Ushindani wa kibiashara na vyombo binafsi katika usafirishaji katika barabara zinazozunguka maziwa yetu.
iv) Gharama na kodi zilizowekwa na Serikali kama ushuru wa mafuta, gharama za matumizi ya maji ya Ziwa, ushuru wa Serikali za mitaa, na gharama za Mamlaka ya Uthibiti wa Vyombo vya Majini na Nchi Kavu (SUMATRA).
v) Maslahi madogo kwa watumishi ikiwa ni mishahara na posho mbalimbali ambazo zinafanya baadhi ya watumishi kukimbilia kwa washindani wetu kwa visingizio vya kufuata maslahi bora zaidi.

vi) Kuzorota kwa utendaji wa reli katika kusafirisha abiria na mizigo wakati wa kipindi cha mpito kuelekea ubinafsishaji kuliathiri sana utendaji wa meli zetu.
vii) Kupungua kwa kina cha maji katika maziwa yetu kuliathiri uwezo wa upakiaji wa mzigo katika kiwango kinachohitajika na vile vile kuathiri usalama wa meli zetu.
viii) Kuchakaa kwa miundombinu ya kibandari katika maziwa yetu na sehemu nyingine kutokuwepo kabisa, kumeathiri utendaji wa meli zetu katika kubeba abiria na mizigo.
ix) Kutokuimarika kwa hali ya kisiasa Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuliendelea kukwaza shughuli za kibiashara na usafirishaji wa abiria.
x) Majukumu ya kuendelea kutoa huduma katika maeneo ambayo Kampuni inafanya uendeshaji kwa hasara (Public Obligation) bila kupata ruzuku yoyote toka Serikalini, inapunguza zaidi uwezo wa Kampuni kusonga mbele kimaendeleo.

**Matarajio ya Kampuni**

i. Kujiendesha kwa uwezo wote tulio nao ifikapo mwaka 2013.
ii. Kutoa huduma zenye ongezeko la thamani.
iii. Kuajiri na kubakiza watumishi stadi katika soko la sasa.
iv. Kuongeza mapato ya shughuli kwa zaidi ya 50% ifikapo mwisho wa mwaka 2013.
v. Kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kwa usalama, uhakika na kwa bei nafuu.
vi. Kuwekeza kwenye miradi ambayo inalenga kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha huduma.

## *Tumethubutu, Tumeweza, Tunazidi Kusonga Mbele*